



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU



Unapojibu Tafadhali Taja.

Kumb.Na.MDC/DED/L2/9/VOL.II/29

22/02/2022

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA KUKUSANYA TAARIFA ZA ANWANI YA  
MAKAZI NA POSTIKODI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu anapenda kuwatangazia nafasi za ajira ya muda kwa nafasi za **Wakusanya Taarifa** kwenye zoezi la Anwani za Makazi katika Kata na Vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu.

**A. SIFA ZA MAOMBAJI**

- Awe raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18-35
- Awe na elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea
- Awe anamiliki simu janja android yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa siku nzima
- Awe na barua pepe (email address) na nywila (password) inayofanya kazi
- Awe na uwezo wa kusoma ramani za mitaa
- Awe ni mkazi wa Kata husika.

**B: KAZI NA MAJUKUMU**

- Kugawa / kuandika namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma.
- Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maendeleo ya huduma.
- Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja na maeneo ya huduma kwa kutumia mfumo wa anwani za makazi.
- Kutuma data kwenye mfumo wa anwani za makazi.

**C: MSHAHARA**

Mwombaji atakayeajirwa atalipwa kwa siku kwa muda wa siku atakazofanya kazi.

**NB: MASHARTI YA JUMLA.**

- Ajira hii ina masharti ya Mkataba wa Muda wa siku thelathini (30) na siyo ajira ya Masharti ya Kudumu
- Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wawe wakazi wa kawaida wa Kijiji na Kata husika katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, wenye umri wa kuanzia miaka 18 hadi 35.

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, S.L.P 74 Mbulu-Manyara, Simu +255-027-2975124, Nukushi +255-027-2975124, Barua pepe [md@mbuludc.go.tz](mailto:md@mbuludc.go.tz). Tovuti [www.mbuludc.go.tz](http://www.mbuludc.go.tz)

- iii. Barua ya maombi ipitie kwa Mtendaji wa Kijiji na Kata anapoishi
- iv. Maombi yote yaambatanishwe na nakala ya cheti cha kuzaliwa; vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kidato cha nne na/au kidato cha sita na kuendelea kwa wale waliofikia kiwango hicho
- v. Maombi yaambatane na Picha mbili "Passport size" za hivi karibuni na ziandikwe majina ya mwombaji kwa nyuma.
- vi. **Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 28 Februari, 2022 saa 9.30 mchana.**

**Tangazo hili linafuta Tangazo lenye Kumb.Na.MDC/DED/L2/9/VOL.II/28 lililotolewa tarehe 21/02/2022.**


#### **D:JINSI YA KUTUMA MAOMBI**

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, namba ya simu na barua pepe na ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri kwa anuani ifuatayo:-

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA MBULU  
SLP 74  
MANYARA.**

Tangazo hili pia linapatikana kupitia tovuti ya Halmashauri [www.mbuludc.go.tz](http://www.mbuludc.go.tz)

Tangazo hili limetolewa na;

  
Abubakar A. Kuuli  
Mkurugenzi Wa Halmashauri  
Halmashauri Ya Wilaya ya Mbulu.

---

**Nakala:**

#### **Mbao za Matangazo zote:**

1. Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu (Makao Makuu, Hospitali ya Kilutheri Haydom, Ofisi za Kata/Vijiji, Makanisa, na Misikiti
2. Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji, Halmashauri ya Mji wa Mbulu
3. Ofisi ya Katibu Tawala, Wilaya ya Mbulu

---

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, S.L.P 74 Mbulu-Manyara, Simu +255-027-2975124, Nukushi +255-027-2975124, Barua pepe [md@mbuludc.go.tz](mailto:md@mbuludc.go.tz). Tovuti [www.mbuludc.go.tz](http://www.mbuludc.go.tz)